# *Wakati Wa Uamuzi*

Asante, ndugu.

2 Asanteni. Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu sasa katika maombi.

3 Bwana, tunashukuru kwa ajili ya wakati huu mzuri wa ushirika ambao tumekusanyika hapa katika Kanisa hili la Philadelphia huku Chicago, si kwa sababu yoyote nyingine ila kukuheshimu na kukuthamini Wewe, na kukuabudu Wewe kwa moyo wetu wote. Nasi tungeomba, Bwana, ya kwamba Wewe ungekutana nasi usiku wa leo kwa njia maalum sana, ukitupa shauku ya moyo wetu, kama ni mapenzi Yako, Bwana.

4 Nasi tunaamini ya kwamba kama tutatembea kwa unyofu mbele Zako, kwamba Wewe hutatuzuilia jambo lolote jema. Kwa hiyo tunaamini ni mapenzi Yako kutubariki usiku wa leo. Tunaomba baraka maalum kwa ajili ya wahudumu walio hapa katika ibada, wamekuja kwenye mkutano kujazwa na mambo mazuri, kwenda nyumbani na mwanzo mpya na sura mpya, ono jipya kutoka kwa Mungu katika kazi Yake na mapenzi Yake.

5 Nasi tunaomba ya kwamba Wewe pia utawakumbuka wagonjwa usiku wa leo, Bwana, kwa kuwa kuna wengi walio wahitaji, hawana budi kuguswa na Wewe wapate kuendelea, na hasa sana wale walio mahututi sana usiku wa leo wanaopiga simu kutoka hospitalini na kote nchini, tunawaombea.

6 Tunawaombea wale ambao hawako kwenye Njia bado wanaoangalia, jalia huu uwe ndio wakati ambapo watasema, "Naam, Bwana, jalia nijiunge na safu yao." Na waweke kando kila mzigo uwazingao kwa upesi, wapate kupiga mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yao, wakimtazamia Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani, Bwana Yesu.

7 Nisaidie, Bwana, nimechoka usiku wa leo, nami ninaomba ya kwamba rehema Zako zitaonyeshwa kwa mtumishi Wako. Kwa kuwa tunaomba haya, katika Jina la Yesu. Amina.

8 Mnaweza kuketi. [Ndugu Joseph Mattsson-Boze anatoa tangazo—Mh.] (Ni sawa.) Ninauhesabu huu kuwa mmoja wa nyakati kuu sana za maisha yangu, wakati nikiwa na majaliwa ya kusimama mbele ya wale walionunuliwa kwa Damu ya Kristo kuihubiri Injili. Kwa hiyo napenda kuja kwa uchaji, na kwa busara, na kwa kiasi, na katika kumcha Mungu tunapokuja kuzungumza na kusanyiko kama hili, kwa kuwa kuna karibu, nadhani, watu elfu moja hapa, na wengi wa hao ni watakatifu waliooshwa kwa Damu.

9 Na huenda kukawa na wale hapa ambao wanajaribu kufanya uamuzi juu ya jambo la kufanya. Kwa hiyo basi sote tunapaswa kukumbuka kuenenda jinsi Wakristo wanavyopaswa kufanya, kwa maana twajua ya kuwa sisi ni nyaraka zilizoandikwa za Mungu, zinazosomwa na watu wote.

10 Sasa, kesho usiku, imetangazwa kwamba tutakuwa na ibada ya uponyaji, hiyo siyo kile tungeweza kuita ibada ya uponyaji, bali ni kuwaombea wagonjwa. Kamwe sijaweza kuliingiza katika nia za watu, sio Kanisa, bali wale walio nje, kwamba hatuwezi kuponya. Kamwe sijapata kumponya mtu yeyote, kamwe sitaponya, bali nimekuwa na majibu halisi ya moja kwa moja ya maombi. Mungu ameyaheshimu maombi ambayo nimeomba mara nyingi. Hivyo ndivyo tunavyotaka kuwafanyia wagonjwa kesho usiku.

11 Nilikuwa na mazungumzo mafupi leo, kamwe nisingeweza kuendelea, dhamiri yangu ilikuwa ikinihukumu, na ikanibidi kuzungumza na Ndugu Grant. Sijamjua Ndugu Grant vizuri sana, lakini nilimwona kuwa mtu wa aina ile niliyowazia alikuwa, Mkristo halisi muungwana, mpole.

12 Lakini hivi majuzi usiku, bila kujua kwamba hata alikuwa mkutanoni, nilizungumza kutoka jukwaani, nikisema, "Usiku mmoja sikuzote tunautenga kwa ajili ya uponyaji. Niliitwa kuzungumza, lakini tutawaombea wagonjwa usiku mmoja, na hebu tuufanye huo Ijumaa usiku." Ndugu Grant, aliyeketi hapa, tayari alikuwa ameutangaza huo kwamba ndio usiku ambapo angefanya mkutano wa Roho Mtakatifu. Na hata hivyo, Ndugu Joseph aliniambia tayari ilikuwa imeeleweka, na kuzingatiwa na Ndugu Grant, bali nilihisi kwamba ilinibidi kumwambia mimi mwenyewe, ya kwamba sikujua hilo.

13 Ni mtu mzuri jinsi gani niliyempata katika Ndugu Grant! Ana mikutano mikubwa katika mikutano yake mwenyewe, naye alitaka kuitoa kwa ajili ya wagonjwa, kuwaombea wagonjwa. Ndugu Grant, kwa unyenyekevu sana, mwenyewe ametumiwa na Mungu katika kuwaombea wagonjwa, na ni mtu mashuhuri sana wa imani. Lakini alikaa muda mrefu sana ibadani wakati mmoja, karibu imwue, yeye ni dhaifu na mwenye wasiwasi, na karibu arukwe na akili, kabisa.

14 Ndugu Tommy Hicks, nasikia, ana mshtuko wa moyo, amefanya kazi kupita kiasi. Loo, kama nilivyosema hivi majuzi usiku: watu wa Mungu wanahitaji mretemu, mapumziko. Hebu na tumngojee tu Bwana, ndipo tufanye upya nguvu zetu tunapomngojea; usijaribu kufanya yote.

15 Ninakumbuka nikikaa kwenye mstari wa maombi kwa siku saba mchana na usiku, huku nikila chakula changu mimbarani, nimeyakinia ningemwombea kila mmoja aliyekuja kabla sijaketi. Kulikuwa na mara kumi zaidi kwenye usiku wa mwisho kuliko walivyokuwa nilipoanza; basi karibu nife. Nisingeweza

kulala, karibu sikujua mahali nilipokuwa, nilikuwa nimechoka sana na dhaifu. Haifaidi kufanya hivyo, Yesu hataki tufanye hivyo, anatutaka tujitunze.

16 Hakuna mtu anayejua yale maono hayo hunifanyia mimi, ni magumu sana kwangu. Na kama ingeweza tu kuwa ni mmoja, halafu hao wengine wawe sawa, lakini ukininii. . .ni mmoja, haina budi kuwa ni wote, la sivyo hawataki kuliamini.

17 Kwa hiyo kanisa haliko katika hali yake nzuri bado, inatubidi kukumbuka hilo, halijakomaa. Kwa hiyo inatubidi tu kulimatia na kufanya vizuri tuwezavyo. Wala hakuna mtu anayeweza kulifikisha kwenye ukomavu, ila tu Roho Mtakatifu, tunapomsikiliza. Siamini kamwe utakuja kwa njia ya mwanadamu, itabidi uje kwa njia ya Mungu.

18 Lakini kesho usiku, Bwana akipenda, tutawaombea wagonjwa. Nami nitamtuma Billy, mwanangu, na asipokuja, basi Gene ama Leo, mmoja wao, atakuwa akisambaza kadi za maombi, ama Ndugu Sothmann, ninamwona huko nyuma, kutoka Canada, yuko pamoja nasi katika mkutano. Baadhi yao watakuwa wakisambaza kadi za maombi kesho usiku yapata saa kumi na mbili, kwa hiyo haitaingilia ibada iliyosalia.

19 Halafu basi, Jumamosi usiku, nilisikia jambo hili tangu nilipokuja, kwamba Ndugu Osborn, rafiki yangu wa thamani, anaonyesha sinema yake hapa mjini. Nadhani imetangazwa kutoka hapa. Nayo itaonyeshwa Jumamosi usiku kwenye ukumbi huu wa sinema, ama ukumbi wa shule, nami ningewaomba ninyi nyote mwende mkaione hiyo. Tommy Osborn ni mmoja wa Wakristo waungwana wazuri sana niliopata kukutana nao, yeye ni mtumishi wa kweli wa Kristo, halisi, nami nina heshima kubwa na upendo kwake.

20 Na kwa kuwa niko hapa mjini, basi na—na—nataka kwenda Jumapili alasiri, mimi mwenyewe, kuona hiyo sinema. Lakini kesho usiku, ninasafiri maili nyingi, nyingi sana kwenye kanisa lingine, nilikusudia kusema Jumamosi usiku, kwenda kwenye kanisa lingine kwa ajili ya ibada ndogo. Labda kuhubiri tu kwenye. . .mahubiri madogo kisha nirudi, kwa sababu ni kanisa fupi, au, kanisa dogo, hakuna wengi wanaoweza kuingia, linahusishwa na kanisa hili. Na kisha Jumapili alasiri, ninakusudia kuiona hiyo sinema, mimi mwenyewe.

21 Halafu basi, Jumapili usiku, ni ibada nyingine, na katika ibada hiyo, tutawaombea wagonjwa tena, Bwana akipenda, Jumapili usiku kwenye ukumbi. Mchungaji wenu hapa aliniambia asubuhi ya leo tulipokuwa tukizungumza, akiwa na roho ya kishujaa sana, alisema ya kwamba angefunga kanisa hili, kwamba hawatakuwa na ibada kwenye Kanisa la Filadelfia wakati tukiwa mjini, tukiwaombea wagonjwa. Huo ni ushujaa mkuu, tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo, kwa ajili ya Ndugu yetu Ead aliyeniambia jambo hilo asubuhi ya leo.

22 Jumamosi asubuhi ni kiamshakinywa cha Wafanyabiashara Wakristo. (Nadhani hiyo imepangwa.) Ime—imepangwa. Halafu nafikiri kesho asubuhi ni kiamshakinywa cha wahudumu. Na hicho kinafanyiwa kwenye Sheridan Plaza. Na cha Wafanyabiashara Wakristo? Ufuko wa Edgewater. Na kwa hiyo, ninaamini ninakusudiwa kuzungumza kwenye ibada hizi zote mbili.

23 Kwa hiyo, Bwana awabariki sasa tunapoomba baraka Zake juu ya kusomwa kwa Neno, na kwamba atatupa usiku wa leo Roho Wake.

24 Sasa hebu na tuweke kando kila masumbuko na wasiwasi wa siku hizi. Hakuna wasiwasi, tupilia mbali kila kitu, na sasa umtazame Yeye kwa dakika thelathini ama arobaini zijazo.

25 Bwana, tuna furaha ya kwamba tunalo Neno lililo hai na Neno lililoandikwa, Nayo yanashuhudiana Moja na Lingine. Hilo linatufanya tuwe na hakika ya kwamba tunaposoma Biblia hii iliyobarikiwa, kwamba ni changamoto kwetu. Nasi tunajua Yule aliyeliandika yupo, yupo daima kufanya kila Neno kuwa kweli na sahihi. Kwa hiyo, lizamishe Neno usiku wa leo, kwenye kilindi, ndani ya mioyo ya watu kwa Roho Mtakatifu, limwagilie maji kwa maungamo na toba lipate kustawi likawa miti mikubwa ya wokovu, kusudi wanaume na wanawake wakaidi wapate kuja chini ya matawi yake na kupumzisha nafsi zao. Jitwalie Mwenyewe utukufu. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

26 Ninataka kuchukua fungu usiku wa leo linaloitwa hivi: *Wakati Wa Uamuzi*. Ninataka kusoma kutoka Mwanzo 24:58, kifungu kimoja tu:

> *Wakamwita Rebeka, wakamwuliza, Je, utakwenda na mtu huyu? Akasema, Nitakwenda.*

27 Mnajua, tumelazimika kufanya maamuzi, kuna nyakati ambapo inatubidi kufikia mahali ambapo tunapaswa kusema *ndiyo* au *la*, hiyo ni katika maisha ya mwanadamu tu, upo wakati ambapo hatuwezi kusimama bila kuchukua upande wowote. Na kama Mungu akiruhusu, siamini ya kwamba tutaweza kuondoka kwenye kanisa hili usiku wa leo katika hali zile zile tulizokuwa nazo tulipoingia humu. Ikiwa Roho Mtakatifu atakuja na kufanya kazi Yake miongoni mwetu, basi tunalazimika kusema *ndiyo* au *la*, hatuwezi kubaki vile vile.

28 Basi wakati ulikuwa umewadia kwa Ibrahimu, yule mzee mkuu, na mtumishi wa Mungu, kufanya uamuzi. Na uamuzi huu ulikuwa, kwamba alipaswa kuamua ni nani mwanawe, Isaka, ambaye alikuwa amemngojea miaka ishirini na mitano, na alikuwa amempokea kama mtu kutoka kwa wafu, na alijua ya kwamba yeye mwenyewe alikuwa ni mjumbe wa Mungu aliyeitwa na kutengwa, na kulikuwa na wakati uliokuja ambapo

ilimbidi kuamua: Ni nani angekuwa msaidizi wake kuendeleza mpango wa Mungu?

29 Mnaona, Mungu hafanyi maamuzi yetu yote. Na kuna mara nyingi ambapo Mungu hawaambii manabii Wake la kufanya, kwa sababu inawabidi kufanya uamuzi. Kama hakuna uamuzi tunaopaswa kufanya, ni kumngojea tu Mungu kwa kila hatua, basi hakuna ushindi kwetu. Na wakati mwingine, wanafanya uamuzi mbaya, Manabii wa Mungu waliotiwa mafuta hufanya maamuzi mabaya, na mara nyingi wanadanganyika.

30 Hivi uliwahi kuwazia juu ya Isaka, wakati Esau na Yakobo walipomjia huyu nabii mkuu wa Bwana, ameketi pale kipofu kimwili, na wakati huo, kipofu kiroho? Naye Yakobo alikuwa amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo shingoni na kuvaa koti la Esau, apate kunuka kama makondeni, naye baba yake, huku amemwekea mwanawe mikono yake ya kinabii, alidanganywa kiroho na mwanawe, ingawa alikuwa ni nabii.

31 Vipi Elisha, mtu mwenye nguvu wa Mungu. . .? Wakati yule mwanamke Mshunami alipoingia ndani haraka, akilia, Elisha alijua ya kwamba alikuwa anasumbuka, naye akasema, "Mungu amenificha jambo hili."

32 Kwa hiyo wakati umetengwa kwa kila mtu kufanya uamuzi wake, awe mhubiri, ama nabii, ama mfuasi wa kanisa, ama yeyote yule, hana budi kufanya uamuzi.

33 Ndipo wakati huu ukawadia, naye Ibrahimu akaazimia kwamba hakutaka mwanawe aoe asiyeamini. Huo ungekuwa ni uamuzi mzuri kwa Wakristo siku hizi, ambao ni wana na binti za Ibrahimu, kufanya uamuzi uo huo kuhusu watoto wao. Sasa, haikuleta tofauti yoyote jinsi hao wasichana wasioamini walivyokuwa warembo, na jinsi walivyokuwa wanawake wazuri, bali Ibrahimu hakutaka mwanawe ahusishwe na upuuzi kama huo, na kwa hiyo ilimbidi kufanya uamuzi juu ya yule anayepaswa kumwoa.

34 Ndipo wakati ukawadia ambapo ilimbidi kufanya uamuzi juu ya amtume nani kumchagua huyu bibi-arusi kwa ajili ya Isaka, basi wakati huo ulipowadia, aliwaangalia watumishi wake wote. Nasi tunajifunza hapa ndani somo zuri la Ibrahimu, mfano wa Mungu Baba akimtafuta mtumishi aende akamtafutie Mwanawe Bibi-arusi. Hivyo ndivyo Baba anavyofanya siku hizi, analichunguza kundi Lake apate kuona mtu ambaye anaweza kumtumainia, ambaye atachukua Ujumbe ambao Yeye anampelekea Bibi-arusi.

35 Ndipo akaamua kwamba Eliezeri ndiye aliyechaguliwa, kwa sababu alikuwa ameona Eliezeri ni mtumishi mwaminifu, alikuwa mtiifu, na mkweli, na mnyofu, na mwenye haki, na mwaminifu. Huyo ndiye aina ya mtumishi ambaye Mungu anaweza kumchagua kulipelekea Kanisa Ujumbe kutoka Kwake, kama mtu ambaye amethibitishwa kuwa ni mwenye

haki. Mnakumbuka somo langu mara ya mwisho hapa juu ya kuchagua, ama kuwekwa kwa mwana mahali pake, jinsi ambavyo kwanza alithibitishwa, kisha akafanywa mwana mwenye mamlaka katika familia, ama kuwekwa, mahali pake?

36 Basi Eliezeri alitimiza masharti ambayo Ibrahimu alikuwa anahitaji. Naye Ibrahimu anamwakilisha mtumishi kielelezo; mmesoma hiyo hadithi katika Mwanzo 24, jinsi ambavyo hakwenda mpaka alipotumwa.

37 Kuna wengi wanaoenda kwa ajili tu ya pesa wanazoweza kupata kutoka kwake, kuna wengine wanaoenda wapate kujifanyia jina kuu, kuna wengine wanaoenda wapate kuwa maarufu, kuna wengine wanaoenda kwa sababu kwamba mfumo wa huduma fulani wa kujibunia umewatuma, lakini kuna wengine ambao watangojea mpaka Mungu awatume, mtumishi kilelelezo atafanya hivyo.

38 Basi angalieni, alipoenda, alienda tu alikotumwa, si kuja tu *huku* kwa sababu kuna pesa nyingi zaidi, ama *hapa* chini kwa sababu kuna umati mkubwa zaidi, alienda mahali hasa alipotumwa. Mungu anawatafuta watu siku hizi ambao watasonga mbele Roho atakaposonga, mahali popote ambapo Yeye anaweza akawatuma, huyo ni mtumishi kielelezo.

39 Isitoshe, bali alipofika mahali pake ambapo ujumbe wake ulipaswa kutolewa, kamwe hakujigamba, kamwe hakusema jinsi alivyokuwa mkuu, ama jinsi mikutano yake ilivyokuwa mikuu, ama jinsi jambo lolote kumhusu yeye mwenyewe lilivyokuwa kubwa, hakujaa majivuno wala kiburi, bali alinena tu juu ya bwana wake, na juu ya utajiri wa bwana wake, na kwamba bwana wake alikuwa na mwana ambaye alikuwa anaenda kuwa mrithi wa kila kitu alichokuwa nacho bwana wake.

40 Ni picha nzuri jinsi gani ya mtumishi halisi wa Mungu! Umakinifu wake wote uko kwa Bwana, akiwaambia watu, si juu yake mwenyewe, bali juu ya Bwana, na juu ya Mwana, Naye atarithi vitu vyote. Ana muda mwingi sana wa kuzungumza juu ya Bwana na Mwanawe, hata hana wakati wa kujivuna, ama ninii yake—ama huduma yake kuu, ama dhehebu lake, ama ushirika fulani alio nao, yote ni juu ya Bwana wake.

41 Sasa, Eliezeri alikabiliwa na tatizo kubwa kama wahudumu walivyo siku hizi. Kulikuwako na kundi zima la wanawake ambao angeweza kuchagua kutoka kwao, na hilo chaguo ilibidi lifanywe haraka.

42 Hatuna wakati wa kuketi hapa na kuliwazia au kushangaa, hatuna budi kufanya uamuzi upesi, wakati umewadia. Huenda hawa ni watu wanaoketi hapa usiku wa leo, huu utakuwa ndio wakati wako wa mwisho kufanya uamuzi wako, ni wa dharura. Usibahatishe ya kesho, huenda kesho yako isije.

43 Kama vile yule mwanamke wakati mmoja, alikuwa na wanaume wawili ambao alikuwa. . .alidhani alikuwa

anawapenda, wala hakujua aolewe na yupi. Naye angewazia kidogo angeolewa na mmoja, halafu akawazia angeolewa na huyo mwingine. Basi akaahirisha uamuzi wake kwa muda mrefu sana akawapoteza wote wawili. Afadhali tuangalie. Uamuzi hauna budi kufanywa haraka.

44 Halafu tena, huyo mtumishi hakuridhika hapa na kwenda tu, alitaka namna fulani ya hakikisho. Naye akaendelea kuhoji, "Vipi kama mwanamke huyo hatakuja? Nitakapomwambia mambo haya, vipi kama hatakuja? Nini basi?" Ndipo ilimbidi kufanya uamuzi.

45 Ndipo aliposikia kutoka kinywani mwa bwana wake: "Malaika wa Mungu atakutangulia," loo, napenda tu hilo sana, linalingana kabisa na hoja yangu papo hapo, "Malaika wa Bwana atakutangulia, Naye atamshawishi." Mungu alimtuma Malaika Wake pamoja na mjumbe Wake.

46 Mungu hufanya hivyo, mwajua, hivyo ndivyo afanyavyo; alimtuma Danieli, akawatuma wengine, na akamtuma Malaika pamoja nao. Kwa hiyo, Yeye hufanya jambo lile lile kila wakati, kwa kuwa ndiyo njia Yake ya kunena.

47 Naye akasema, "Malaika…Malaika wa Mbinguni atakutangulia." Loo, naam, kuna wakati ambapo una maamuzi magumu ya kufanya, kuna wakati ambapo wewe, labda katika umri wako wa makamu, una mapato yako ya mwisho, na umeweka kidogo *hapa*, na kidogo *pale*, lakini sasa umefikia mahali, labda, ambapo pesa hizo hazina budi kuwekezwa mahali fulani, inakubidi kufanya uamuzi utaweka wapi pesa hizo. Basi kabla hujawekeza pesa hizo, kwanza, utatafuta mahali ambapo zinawekwa salama.

48 Loo, tuna vitu siku hizi ambavyo ni vya lala maskini amka tajiri, "Wekeza *hapa*, na kesho wewe ni milionea." Lakini usingeweka pesa zako mahali kama hapo, kwa sababu ni mapato ya maisha yako. Lakini utafanya nini? Kwa kiasi na uaminifu, utatafuta kampuni ya kale, inayoaminika ambayo imejaribiwa na kuthibitishwa, ambayo ni salama, na humo utawekeza pesa zako, kwa sababu hutaki bahati nasibu yoyote.

49 Na kama wewe ni mwaminifu hivyo na unajali katika uamuzi wako kuhusu mapato ya maisha yako, ni zaidi sana vipi unavyopaswa kuwa mwaminifu zaidi kuhusu dini yako na wokovu wako? Hatupaswi kufuatilia baadhi ya mawazo haya ya bahati nasibu, ama kuandika jina lako kwenye kitabu cha kanisa, na kupeana mikono na mhubiri, hilo halitafaa kitu.

50 Nitawapendekezea, usiku wa leo, Shirika la kale linaloaminika, lililoanzishwa kwenye Siku ya Pentekoste, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka kuishi miongoni mwa wanadamu. Ndilo Shirika linaloaminika sana nilijualo la kuwekeza nafsi yako na maisha yako ya usoni katika Umilele, katika tukio la Kipentekoste la mtindo wa kale, limejaribiwa

kwa muda na kuthibitishwa kuwa ni kweli, miaka elfu mbili haijalibadilisha hata kidogo. Na mgawo ule ule wa faida uliolipwa huko Pentekoste ungali unalipwa na Shirika hili: karama za Roho Mtakatifu, nguvu za uponyaji, kuona maono, Malaika kuwatokea. Na huduma waliyokuwa nayo mitume, iliyowavusha salama, itakupeleka kwenye Kikomo cha nafsi yako salama tu kama ilivyowafikisha.

51 Siwezi kuaminisha mapato yangu ya maisha, kama ningekuwa nayo, juu ya bahati nasibu; wala sitaki yoyote ya madhehebu haya madogo yaliyochipuka huku katika siku hizi za mwisho, na jina langu kwenye gazeti, ama namna fulani ya mhemko mdogo, ninataka tukio la kale linaloaminika. Fanya uamuzi wako wa kufanya maungamo thabiti, na ungoje mpaka utakapopata ujuzi huo wa kukupeleka katika Umilele.

52 Ulikuwa mzuri kwa Paulo na Sila. Ulimfaidi Petro usiku ule gerezani, kesho yake, alipaswa kukatwa kichwa, ndipo Malaika wa Bwana akaja kama Nguzo ya Moto, akamgusa, na kumkomboa. Malaika yuyo huyo angali katika hali ya—ya kutumika usiku wa leo, angali anaambatana na Shirika la Roho Mtakatifu na Kanisa la Mungu aliye hai.

53 Malaika yule yule wa Mungu aliyekuwa pamoja na Paulo kwenye bahari yenye dhoruba, usiku huo ambapo pepo wangemzomea na kumcheka kwa kila mpigo wa radi uliomulika kwenye mawimbi. Alitoka huko mbio akiwa na hakikisho, naye akasema, "Malaika wa Mungu, ambaye mimi ni mtumishi Wake, amesimama karibu nami, hakuna mtu atakayepotea kwenye meli hii."

54 Ningekupendekeza kwenye Shirika hilo, Hilo linaaminika, ni salama. "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia, wakawa salama." Jiweke tu katika akaunti hiyo usiku wa leo, Mungu atawashughulikia walio Wake. Hiyo amana ni salama, imeambatanishwa na Malaika, na ina ishara, na maajabu, na maono, na inaonyesha ushuhuda wa moja kwa moja wa kufufuka kwa Bwana Yesu. Naam.

55 Ninaitaka, hiyo dini ya kale, "Inanifaa vya kutosha, ilimfikisha baba yangu mzee, ikawafikisha Paulo na Sila." Ilimfanya Paulo, wakati walipokuwa wanataka kukikata kichwa chake, kusema, "Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda; na baada ya hayo, nimewekewa taji ya haki ambayo Bwana, Hakimu mwenye haki, atanipa." Ninaipendekeza sana imani hiyo.

56 Kama uko chini ya maamuzi usiku wa leo, na bado hujaamua kama wewe ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mpentekoste, ama Mpresbiteri, hebu niwajulishe ile dini ya zamani, kwa kuwa ni nzuri. Unaweza kutuliza hakikisho la nafsi yako kwamba Yeye atakuvusha.

57 Eliezeri, alipohakikishiwa ya kwamba Malaika alikuwa anamtangulia, basi angeweza kuamua kwenda, kwa sababu alikuwa na kitu cha kumwunga mkono. Nafikiri hilo linapaswa kuwa hakikisho la kila mtu wa Mungu anayeihubiri Injili, kwamba ana kitu cha hakika kutoka kwa Mungu ambacho kitaunga mkono yale anayohubiri. Kama hamjakipata, ndugu, ni kwa ajili yenu, Mungu angali anawatuma watu Wake akiwa na Malaika mbele yake wakati anapoenda kupeleka ujumbe kanisani.

58 Isitoshe, bali wakati Eliezeri alipoondoka, baba yake Isaka, ambaye alimwakilisha Baba yake Kristo, alipakia kundi zima la ngamia zawadi nzuri kwa ajili ya bibi-arusi. Loo, ninajisikia kubarikiwa sasa hivi. Loo, jinsi ninavyompenda Yesu! Alipakia ngamia waliojaa zawadi nzuri za kumpa bibi-arusi, wala kamwe hakumwambia ya kwamba zilikuwa kwa ajili ya kizazi kingine ama siku nyingine, bali zilikuwa ni kwa ajili ya bibi-arusi.

59 Na kila mtumishi wa kweli wa Mungu aliyetumwa ana Kitabu kizima kilichojaa ahadi za Kiungu ambazo anaweza kumtolea Bibi-arusi. Nina furaha sana kwa jambo hilo. Anazo zawadi mle ndani kwa ajili Yake, wala hatazuilia hata moja, atampa kila moja bure, mtumishi wa kweli, mtumishi kielelezo, mtumishi ambaye Mungu anaweza kumtumainia. Hatajaribu kumficha, kwa sababu anajua ya kwamba Yeye ndiye Malkia ajaye.

60 Loo, hakuna kitu chema kinachozuiliwa kwao watakaotembea kwa uaminifu mbele Zake. "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa." Hicho Kitabu kimejaa hayo, na kila ahadi katika hicho Kitabu ni yako, wewe Bibi-arusi.

61 Alikuja kisimani wakati wa jioni. Sasa, ilifikia wakati ambapo ilimbidi Eliezeri kufanya uamuzi mwingine, ilimbidi kufanya uamuzi kama angeamini maoni yake mwenyewe juu ya mwanamke huyo, au angeamini maoni ya Mungu juu ya mwanamke huyo?

62 Loo, jinsi watumishi wa kweli wanavyochanganyikiwa sana na jambo hilo! Wataangalia kote kwenye kanisa fulani kubwa, zuri, Yezebeli aliyejipaka rangi, na kusema, "Hapo ndipo Bwana anaponiita," kwa sababu wasomi wao wamesema Dk. *Nanii* anahubiri huko. Acha Mungu aseme nawe, chukua uamuzi wa Mungu kwamba atakuwa ni nani, ni nani utakayefanya ushirika naye. Sijali ni kwenye kiwango gani, njoo hata hivyo, acha Mungu anene.

63 Basi ilikuwa ni wakati wa jioni wakati alipofika kwenye kisima karibu na mji. Na ilikuwa yapata wakati huo ambapo ilimbidi Rebeka kufanya uamuzi. Ninaamini Malaika wa Bwana alimtangulia pale kwa karibu nusu saa, kwa kuwa atawatuma

Malaika Wake mbele yako, wanaifanya njia kuwa wazi. Na hapana shaka ilikuwa ni Malaika wa Mungu aliyenena na moyo wa Rebeka, kasema, “Nenda ukachote maji.”

64 Naye Rebeka akaja kwenye maji ya uzima wakati wa jioni. Mnaipata picha hiyo? Ni Kanisa katika siku za mwisho, wakati wa jioni, Nuru za jioni ziko hapa. Ni wakati ambapo Malaika wa Bwana katika mambo ya kimbinguni, anajifunua Mwenyewe kwa Rebeka, Bibi-arusi wa Isaka, na *kwa namna fulani*, ameondoka kwenda kwenye Maji ya Uzima. Amina. Loo, moyo wangu unapinduka kwa furaha! Ni vigumu kwangu kuhubiri ninapowazia hilo. Wakati wa jioni umewadia, Malaika wa Bwana yuko katika Ujumbe, anatoka anaenda na kumsihi huyo Rebeka aje kwenye Maji ya Uzima, matendo ya kimbinguni.

65 Eliezeri akaanza kuomba, “Ee Bwana Mungu, jalia jambo la kimbinguni litendeke.” Loo jamani! “Ulimtuma Malaika Wako mbele yangu, sasa hebu na afanye jambo fulani, ninajua Yeye amenitangulia. Na iwe kwamba msichana atakayekuja na kunipa maji kutoka kwenye mtungi, na pia atawanywesha ngamia wangu bila kuombwa, huyo na awe ndiye.” Mara aliposema hivyo, Rebeka akaja. Mungu kamwe hachelewi.

66 Si zaidi ya vile moyo wako unavyomwonea Mungu njaa na kiu, namna fulani ya uamsho wa Roho Mtakatifu utatokea mahali fulani, jambo fulani litatukia, jirani ataponywa na aje akwambie habari zake, jambo fulani litatukia kukufanya uone ya kwamba Malaika wa Bwana anatenda kazi.

67 Kwa hiyo, kwa nini Rebeka akachukua hatua hiyo ya ghafla? Kwa nini akaenda kwenye maji ya uzima upesi hivyo? Kwa nini Malaika angeweza kuzungumza naye? Kwa sababu alikuwa na uhusiano wa damu na Isaka. Na hao ndio Malaika anaoweza kuzungumza nao usiku wa leo ni walio na uhusiano wa Damu, kwa Damu tunazaliwa katika Mwili wa Kristo. Rebeka alikuwa binamu wa Isaka kwa baba wote wawili, jambo ambalo liliwafanya kuwa na uhusiano wa damu. Naye Bibi-arusi wa Yesu Kristo ametakaswa kwa Damu ya Kristo, na chombo wazi cha kuzungumziwa na Roho Mtakatifu. Si ajabu atakuja kwenye Maji ya Uzima. “Yeye asikiaye, na aje kwenye Maji ya Uzima bure.”

68 “Bibi-arusi alisema, ‘Njoo.’ Yeye aliye na kiu, na aje. Heri ninyi mnapokuwa na njaa na kiu ya haki, maana mtashibishwa.” Ni ahadi ya Baba.

69 Alifanya maamuzi yake haraka. Mwangalie Mkristo halisi mkutanoni, upesi, kama wamekusudiwa Uzima wa Milele, watajua jambo hilo, kuna kitu fulani katika ujumbe kinachowachochea. Hicho ndicho kilichomchochea Rebeka, ujumbe ulimchochea, Malaika alikuwa akimwongoza. Loo, hivi hamwezi kuiona hiyo picha? Malaika wa Bwana akimwongoza, ndipo akachochewa, na mara alipowanywesha

ngamia maji, zawadi zikamwendea. Akaanza kutoa hereni, ambalo linamaanisha imani chanzo chake ni kusikia, mnaona, akavalishwa vikuku, kazi za mikono yako, akamweka tayari mara alipoanza kuwapa maji, kuwapa Maji ya Uzima, kushuhudia, kuwaambia wengine, kueneza Ujumbe, kuwaambia yaliyokupata.

70 Ndipo kulikuwa na uamuzi mwingine mkuu uliopaswa kufanywa. Basi baada ya yeye kupewa, ndipo wazazi wake wakasema, "Vema, ningetaka, hebu tumwache akae huku siku kumi. Mwacheni akae kwenye uamsho apate kujisikia kama kweli ameamua kufanya hivyo au la." Sina imani sana na mtu anayefanya uamuzi wa kungojea mpaka kesho.

71 Lakini huo ujumbe ulikuwa umemchochea Rebeka, aliridhika huo ujumbe ulitoka kwa Mungu.

72 Kwa hiyo, wazazi wakasema, "Loo, hebu akae huku kidogo. Atauvuka, ni msisimko mdogo tu, alikuwa huko kwenye uamsho huo, mwajua."

73 Lakini, loo, ndipo yule—yule mtumishi wa kweli akasema, "Usi—usituchoshe, usinizuie." Watumishi wengi wa Mungu wamezuiliwa na maamuzi ya kuahirishwa. "Msinizuie, kwa kuwa Bwana amenituma, kwa kuwa Yeye amekuwa mwema kwangu. Msinizuie."

74 Ndipo wakasema, "Mwache ajiamulie mwenyewe." Hapo ndipo unaposimama usiku wa leo, kufanya uamuzi wako mwenyewe.

75 Ndipo wakamwita Rebeka, na kusema, "Je, utaambatana na mtu huyu, ama unataka kukaa hapa kwa muda kidogo uone kama kweli unataka kufanya hivyo?"

76 Akasema, "Nitaenda." Alikuwa tayari, uamuzi wake ukafanywa upesi. Alijua ya kwamba Kitu fulani kimekuwa kikimwongoza, alijua jambo fulani lilikuwa limempata, naye alijua ya kwamba ilikuwa ni Mungu, naye akaridhika. Alitaka kwenda haraka, kwa hiyo akavaa mavazi yake, naye akachukua zawadi zote alizotumiwa na baba yake kumlaki mwanawe. Ee Mungu, laiti Kanisa lingeweza tu kufanya uamuzi huo upesi sana! Akavaa zawadi zake zote, akapanda juu ya ngamia na kuondoka.

77 Basi ilikuwa ni wakati wa jioni wakati Isaka alipokuwa ametoka hemani kwenda makondeni kutafakari. Ndipo alipowaona ngamia wakija, Rebeka akamwangalia, na ilikuwa ni upendo wa kuonana kwa mara ya kwanza. Ilimbidi kuamini kabla hajaenda. "Imani chanzo chake ni kusikia." Hakujua sura ya mtu huyo, wala haikuleta tofauti yoyote, ilikuwa ni Mungu akifanya maamuzi.

78 Sijali kama Yeye ni mkubwa au mdogo, ana rangi gani, hilo haliniletei tofauti yoyote, Yeye ni Bwana wangu. Nitampenda

nitakapomwona, kwa sababu Yeye ni Zawadi ya Mungu kwangu na kwako.

79 Akashuka kwenye ngamia, naye alikuwa na utaji usoni mwake. Ndipo macho yake mazuri yalipoyaona macho ya Isaka, huyo akaingia mikononi mwake, na kumpeleka nyumbani mwa mama, ama, nyumbani mwa baba na kumwoa.

80 Ndugu, sikiliza, hakuna wakati wa kukawia, ni wakati wa kufanya uamuzi. Ujumbe huu umeleta matokeo ya namna gani kwako? Uko tayari kusema, "Nitaenda, nitaamka niende kwa Yesu, Yeye atanikumbatia mikononi Mwake"?

> Mikononi mwa Mwokozi wangu mpendwa,
> Loo, kuna hirizi elfu kumi, (kasema yule mshairi).

81 Yuko mikononi mwako usiku wa leo, kama tu alivyokuwa kwa Pilato wa kale, na muda umeenda kuliko unavyodhania. Utafanya uamuzi gani sasa, utakapomwona Malaika Wake akitenda kazi, ukiona Ujumbe ukija? Yesu yuaja upesi, Malaika wa Mungu yupo hapa duniani akiwatangulia watumishi, akifanya ishara na maajabu, kama tu vile Yesu alivyosema angefanya, naye yupo hapa sasa.

82 Fanya uamuzi wako na uje Kwake, huku tukiinamisha vichwa vyetu. Ni wangapi hapa ndani sasa huku wameinamisha vichwa vyao, na Roho Mtakatifu mkuu, Mtumishi wa kweli wa Mungu, anabisha moyoni mwako, na kusema, "Loo, labda nimetegemea sana madhehebu yangu na ndugu zangu, bali nataka kwenda kwa Yesu usiku wa leo pamoja na yote yaliyo ndani yangu. Kidogo nimekuwa tu nikiyapinga mambo ya kimbinguni, ni—nimeshangaa kuhusu Malaika, lakini, loo, Ujumbe huu sasa hivi umeufanyia moyo wangu jambo fulani. Ninahisi kitu fulani kikisukuma ndani yangu ambacho kinaniambia huo Ujumbe ni wa kweli. Singojei hata kesho, singojei zaidi, huu ndio wakati wangu wa kuamua"?

83 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa na macho yamefumbwa, ni wangapi katika kusanyiko hili kubwa mngeinua mikono yenu, na kusema, "Ninafanya uamuzi wangu, uwe mgumu, ama uwe rahisi, kama inamaanisha kuitwa mtakatifu anayejibingirisha, kama inamaanisha kuitwa mlokole au mwendawazimu, nitachukua uamuzi wangu usiku wa leo kukutana na Bwana Yesu. Ninaamini Ujumbe. Ninataka kukumbukwa katika maombi"? Inua mkono wako. Mungu azibariki nafsi zenu shujaa. Yapata dazani mbili, nadhani, katika jengo hili wameinua mikono yao.

84 Ee Bwana, unawaona, na unawajua. Jalia Roho Mtakatifu sasa amlete huyo Rebeka kwenye Maji ya Uzima, ambapo burudisho la kupoza huja, Uwepo wa Mungu utailowesha mioyo yao, nafsi zao, na kuwaletea Uzima mpya na tumaini jipya. Jalia Malaika wa Mungu, ambaye ametumwa kabla ya Ujumbe, anene

kuhusu jamaa wa Damu ambaye amenunuliwa na Kristo wa thamani.

85 Mikono hii yote iliyo hewani, Bwana, jalia wakupokee Wewe kwa utamu na unyenyekevu sasa hivi, na kuwekwa juu ya ngamia, zile nguvu za Mungu zitakazowabeba hadi kwenye Uwepo wa Bwana. Na kila karama njema iliyoahidiwa iwekwe juu yao, jalia karama ya upendo, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, upole, utu wema, saburi, imani, wapewe kutoka katika ile hazina kuu ya Nyumba ya Mungu, Yeye aliyeahidi mambo yote bure kwa hao watakaokuja.

86 Wana uamuzi wao, Bwana, wameinua mkono wao, wameamua usiku wa leo, Nawe unaweza kusema na wale waliooshwa kwa Damu, Wewe unawajua, Bwana. Tunawakabidhi Kwako, ya kwamba kwenye wakati huo wa mkutano, wakati Kanisa litakapokutana na Yesu hewani . . .

87 Nasi tunaamini ya kwamba Yeye tayari ameondoka kwenye Nyumba ya Baba na yuko njiani Mwake kuja duniani, Naye yuko kwenye makonde ya ile Ng'ambo kuu, huko nje makondeni akitafakari, naye Bibi-arusi anajiweka Mwenyewe tayari, na hivi karibuni atakuwa njiani. Maandiko yanasema ya kwamba tutamlaki Bwana hewani. Yeye tayari ameondoka na anakuja kumchukua Bibi-arusi Wake. Na tuwe tayari, kwa kuwa huu huenda ukawa ndio wito wa mwisho. Wakati wa jioni umewadia. Ninawakabidhi mikononi Mwako na kwenye ulinzi Wako, Bwana. Kupitia kwa Yesu Kristo, tunaomba, na kukupa Wewe ishara za Ujumbe. Amina.

Ishara ya mateso na aibu,
Nami ninaupenda ule msalaba wa kale ambapo
 Mpendwa na aliye Mwema sana,
Aliuawa kwa ajili ya ulimwengu wa wenye
 dhambi waliopotea.

Kwa hiyo nitauthamini ule msalaba wa kale
 unaoparuza,
Hata nyara zangu hatimaye nitaziweka chini;
Nitashikilia ule msalaba wa kale unaoparuza,
Na kuubadilisha siku moja na taji.

Nitakuwa mwaminifu kwa msalaba huo wa
 kale unaoparuza,
Aibu na fedheha yake nitaibeba kwa furaha;
Ndipo ataniita siku moja (Mungu abarikiwe!)
 Nyumbani kwangu mbali sana,
Ambako utukufu Wake milele nita-. . .

88 Unalimaanisha? Inua mkono wako unapouimba.

Kwa hiyo nitauthamini ule msalaba wa kale
 unaoparuza,
Hata nyara zangu hatimaye nitaziweka chini;
Nitashikilia msalaba wa kale unaoparuza,

Na kuubadilisha siku moja na taji.

Loo, jinsi ninavyompenda! Loo, nafsi zenu tu zipate kuoga katika wema Wake! Malaika wa Bwana yupo hapa.

. . . mwishowe . . .
Nitaushikilia ule msalaba wa kale unaoparuza,
(Bila kujali kitu kingine chochote.)
Na kuubadilisha ninii . . .

89 Umewahi kuwazia jinsi hilo lilivyo kuu? Ungeweza kutoa nini kubadilisha na hilo katika siku hii ya machafuko, siku hizi wakati watu hawajui la kufanya, wapitie wapi? Biblia ilisema siku hizi zitakuja, na ya kwamba kutakuwa na njaa nchini, si kwa ajili ya mkate na maji, bali kwa ajili ya kusikia Neno la kweli la Mungu. Na kwamba watu wangeenda kutoka mashariki hadi magharibi, kutoka kaskazini hadi kusini, wakitafuta kusikia Neno la kweli la Mungu. Nasi sisi hawa hapa tumejaliwa usiku wa leo kuona Ujumbe wa Mungu, Malaika wa Mungu.

90 Hakuna kadi za maombi zinazotolewa. Hivi kuna kadi zozote za maombi mkutanoni? La. Hakuna mtu aliye na kadi ya maombi. Lakini Malaika wa Bwana yupo hapa. Kama Mungu akituma ninii Yake . . . ? . . . Yeye hutuma Ujumbe Wake kuthibitisha hilo. Mnaamini?

91 Sasa wote walio hapa ndani wasionijua mimi, ama mnajua siwajui, nawe ni mgonjwa na mhitaji, inua mkono wako. Wote mnaojua sijui chochote mnachohitaji, inua tu mkono wako. Kama unamhitaji Mungu, inua tu mkono wako. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

92 Yule ndugu Myahudi, ama, ninaamini kama hiyo ni kweli, kutoka huko Michigan. Awali ulitoka ng'ambo huko Siberia, mahali fulani . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . -slovakia. Ninamjua. Hao karibu ndio wote ninaoona ninaowajua.

93 Lakini kama Mungu angali ni Mungu, kama Mungu angali anamtuma mjumbe Wake pamoja na Malaika, Malaika atashuhudia kwamba ni kweli. Na ijulikane usiku wa leo ya kwamba Mungu angali ni Mungu. Wala sineni kwa shauri langu, bali ninanena habari Zake. Na kama wewe ni Bibi-arusi, yule Rebeka . . .

94 Biblia ilisema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, na wakati alipoguswa katika siku za mwili Wake, Yeye angeweza kugeuka na kumwambia huyo mwanamke shida yake ilikuwa ni nini, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

95 Biblia ina karama nzuri ambazo Baba huwapelekea watoto Wake. Sasa, ninyi . . . Msimwangalie mjumbe, bali aminini Ujumbe, naye Mungu atawafungulia usiku wa leo ahadi Zake,

kwa kuwa ni nzuri vile vile kwako wewe uliyeinua mkono wako kwa ajili ya wokovu, zinakufaa vivyo hivyo wewe ambaye umeinua mkono wako kwa ajili ya ugonjwa. Mungu yeye yule tu, karama zile zile ambazo amekuwa nazo daima, zikifanya kazi vivyo hivyo.

96 Sasa ombeni, aminini. Acha Bwana Mungu aamue, kisha uimarishe imani yako juu ya Neno la Milele la Mungu. Fanya uamuzi wako usiku wa leo kumtumikia Yeye. Bwana Mungu na aonyeshe angalau watu watatu katika jengo hili (Ambapo, tatu ni uthibitisho. Hiyo inatosha?) ya kwamba alimtuma Malaika Wake, wala siyasemi mambo haya juu yangu mwenyewe, ni Yeye. Katika siku hii wakati hujaamua, naomba uamue kwa ajili Yake.

97 Hapa. Kuna maskini mwanamke aliyeketi hapa na leso yake, kamwe hakuitoa mkononi mwake, na akaendelea kuinua mkono wake. Hivi hatufahamiani, ewe msichana, unayeketi hapo ukiomba? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Unakabiliwa na upasuaji. Hiyo ni kweli, sivyo? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sikujui. Kama hiyo ni kweli, inua ninii yako, ama, weka mkono wako namna *hii*. Lakini hiyo ni kweli, sivyo?

98 Unafikiri nini? Je, umefanya uamuzi wako? Vema, dumu nao basi.

99 Huyu hapa mama mkongwe ameketi papa hapa amevaa nguo inayoonekana nyekundu na mikono yake *hivi*. Unaomba, na unamwomba Mungu akuponye. Sikujui, Mungu anakujua. Ikiwa Bwana ataniambia kile unachoombea, utakubali na kuamini ya kwamba Malaika Wake amekuja kwako kukubariki? Kwa maana juu yako inasimama ile Nuru. Una yabisi kavu na wasiwasi. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema. Je, umefanya uamuzi wako? Vema, nenda nyumbani na usahau kuhusu kuwa mgonjwa basi, Yesu Kristo atakuponya.

100 Ninamwona maskini mama mmoja ameketi hapa nyuma, mikono imeinuliwa *hivi*, anaomba, anajikaza. Simjui. Anaota mvi, lakini ana ugonjwa wa moyo anaoombea. Hiyo ni kweli. Huyo ni dada yake aliyeketi karibu naye, naye anaombea ugonjwa wa wasiwasi. Hiyo ni kweli, sivyo, mama? Sikujui, Mungu anakujua. Wewe hutoki kwenye mji huu, hakuna kati yenu, mnatoka Illinois, hata hivyo, Danville. Hiyo ni kweli. Jina lako ni Bi. P-o-g-u-e. Hiyo ni kweli. Nenda nyumbani, utapata jibu lako. Mungu awape nyote wawili . . .

Aminini tu.

101 Je, hilo lilikusisimua, mama, uliyeketi papa hapa ukiniangalia? Nilikuona ukitabasamu. Umevaa maskini nguo ya mirabamiraba, ya waridi. Nilipogeuka, Malaika wa Bwana alikuwa amesimama pale. Unasumbuliwa na ugonjwa wa miguu. Una rafiki unayemwombea, pia, ana pumu. Hiyo ni kweli, sivyo? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Amina.

102 Unaamini? Malaika wa Bwana! Mtu mwingine inua mkono wako, ambaye simjui, nawe unataka Mungu akusaidie. Hiyo ni kila mahali. Hiyo imeninii . . .? Hao wamekuwa zaidi ya watatu, sivyo? Vema. Hilo linapaswa kulishawishi. Mungu yupo hapa, Mungu anawapenda ninyi nyote.

103 Siwezi kujizuia kusema jambo hili: Yupo mama aliyeketi hapa ambaye ni mhitaji sana, ananiangalia. Siwezi . . . Hiyo hapo Nuru imesimama juu ya mwanamke huyo. Unaamini Yeye atakusaidia? Wala wewe hutoki hapa, unatoka Iowa, Des Moines, Iowa. Unaamini ya kwamba Yeye atakuponya? Una ugonjwa wa mapindi. Hiyo ni kweli. Una tabia unayotaka kuacha: kuvuta sigara. Utaiacha? Inua mkono wako, useme, "Nitaiacha, Bwana." Vema, nenda nyumbani, usivute sigara tena, na mapindi yako yamekwisha, kwa sababu imani yako imekuponya. Mungu akubariki, amini.

104 Unaamini kwa moyo wako wote? Malaika wa Bwana huambatana na Ujumbe, sikuzote. Je, umefanya uamuzi wako kwamba Yeye ni Mungu? Basi wekeaneni mikono. Haikubidi kungojea mpaka kesho usiku, acha iwe usiku wa leo. Wakati Roho Mtakatifu aliponena nami dakika chache zilizopita, si— sikungojea mpaka kesho usiku, usiku wa leo ulikuwa usiku wa uponyaji, usiku wa leo ni usiku wa msamaha. Wekeaneni mikono.

105 Yesu, katika Ujumbe Wake hapa kutoka kwa nguvu za Mungu, Neno la Mungu, nina Ujumbe kwa ajili yenu, hapa, nitautoa mfukoni: "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Ni kwa ajili yako, Rebeka. Inasema nini? "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Unaamini Hiyo, Rebeka? Vema, hii hapa karama inakuja, ipokee, ishike, na uiweke kwenye mkoba wako.

106 Bwana Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, kemea kila pepo, na kutoa magonjwa yote, na kumponya kila mtu, kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu.

59-0611 Wakati Wa Uamuzi
Philadelphia Church
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org